JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

# TAARIFA KWA UMMA

## MAHAFALI YA KUMI NA TATU (13) YA WAUGUZI NA WAKUNGA KUFANYIKA 21.03.2025

***12.03.2025, Dodoma.***

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania, anawataarifu wauguzi na wakunga wote waliopata sifa za kusajiliwa na Baraza baada ya kufaulu Mtihani wa Usajili na Leseni uliofanyika **tarehe 20.12.2024** kuwa, Mahafali ya 13 ya kutunuku Vyeti vya Usajili na Leseni yanatarajiwa kufanyika Jijini Dodoma siku ya Ijumaa ya **tarehe 21.03.2025** kuanzia **Saa 01:00 Asubuhi** katika Ukumbi wa Chuo Kikuu cha **UDOM (Chimwaga Hall)** uliopo Jijini Dodoma.

**Aidha**, kila mwanamahafali anatakiwa kuthibitisha ushiriki wake kwa kujisajili kupitia Tovuti ya Baraza *www.tnmc.go.tz* na kuhudhuria bila kukosa.

**Wanamahafali wote mnaelekezwa kuzingatia mambo yafuatayo;**
Kuvaa Sare ya Kitaaluma ***"Professional Uniform"*** iliyoidhinishwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga kama ifuatavyo: -

- **WANAWAKE-** Gauni au Suruali na Blauzi rangi nyeupe ndefu.
- **WANAUME-** Kaunda suti- Shati la rangi nyeupe na suruali rangi ya ***dark blue***
- **VIATU-** Vinavyofunika miguu na siyo vya wazi, viwe vya rangi nyeusi, nyeupe au ***brown.***

Kitambulisho cha Indexing, NIDA au Kitambulisho cha mpiga kura chenye picha ya mhusika/kinachomtambulisha.

***NB:*** *Sandozi au Kandambili haviruhusiwi.*

***Ndimmyake Mwakapiso***
***Mkuu wa kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano TNMC***

@tnmchabari
+255 737 96 26 91
Ofisi ya Msajili TNMC
S. L. P 1736 Dodoma -Tanzania
Simu +255 736 00 60 60
Barua pepe: info@tnmc.go.tz